# Darubini ya Wiki

*Kwa mwenye bongo pevu* | Toleo Nambari 17 | Desemba 25, 2022 NAKALA BILA MALIPO





# NJIAPANDA

**Juhudi za serikali ya Ruto za kufufua uchumi zinatatizwa na ukosefu wa uwiano kati ya sera ya matumizi ya pesa na sera ya usambazaji wa pesa. Hazina ya Kitaifa inaposisitiza kupunguzwa kwa bajeti huku ikitumia pesa katika miradi isiyo muhimu kutokana na msukumo wa kisiasa, Benki Kuu imekuwa ikitaka kupunguzwa kwa usambazaji wa pesa ilhali inaruhusu kuenea kwa mikopo kupitia kwa simu**

# *The Nation ePaper NOW Available on the PlayStore*

# anywhere, anytime.




Follow the link to subscribe

> ***epaper.nation.africa.***

Scan to Download

Or download from Google playstore

ANDROID APP ON Google play

**Nation** (Facebook)

**Nation** (YouTube)

**Nation Africa** (Twitter)

For customer support Tel: 0790 111 111

Email: epaper@ke.nationmedia.com

NATION ePaper

kauli ya mhariri

## Yaliyomo

**6 MWANASIASA ALIYE MBIONI:** Naibu Rais Rigathi Gachagua afuata nyayo za wenzake huku akijitahidi kujenga ngome yake katika Mlima Kenya. Je, atafaulu ilhali wengine walishindwa?

**8 DUALE NA HIJABU:** Waziri wa Ulinzi azua ubishi mkali tena kwa kusisitiza kuwa wasiotaka kuvaa hijabu wanafaa kuondoka nchini.

**11 LA NINA YAHANGAISHA AFRIKA KUSINI:** Maisha yameathiriwa huku mvua kubwa inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ikiponda Johannesburg na maeneo mengine nchini humo.



**13 MKATABA WA AMANI NA MAUMBILE:** Suluhu yapatikana baada ya dunia kufikia mkataba mwingine muhimu kuhusu mazingira katika mkutano wa COP15 jijini Montreal, Canada.

# Kwa nini itachukua zaidi ya kauli mbiu kufikia muujiza wa kiuchumi wa Kibaki

Huu umekuwa mwaka mgumu kwa Wakenya wengi kwa kila hali.

Ukame mkali ulifanya wengi kuumizwa na makali ya njaa, huku makadirio rasmi ya serikali yakionyesha raia wapatao milioni nne wanahitaji msaada wa chakula kwa dharura.

Bei za mafuta zilipanda hadi kiwango ambacho hazijawahi kuuzwa katika historia ya Kenya, na kuathiri uchumi huku bei za bidhaa na huduma zikipanda.

Vita vya Urusi na Ukraine vilivuruga mifumo ya usambazaji na kusababisha kupanda kwa bei za bidhaa nyingi na mali ghafi ambazo zilifanya kiwango cha mfumuko kuzidi kilichowekwa na Benki Kuu ya Kenya cha asilimia 7.5 karibu mwaka mzima.

Nchi nyingi za Afrika, ziliathiriwa vibaya kwa kuwa zililazimika kuchukua mikopo ghali kujikinga na kununua chakula kwa raia wake wanaokumbwa na njaa. Mwezi huu tu, Ghana ilifanya kilichoonekana kutowezekana miaka michache iliyopita.

Nchi hiyo ilisimamisha ulipaji wa madeni ya nje, ikiwemo ya Eurobond, mikopo ya kibiashara na iliyopatiwa na nchi zingine, na hivyo basi kushindwa kulipa madeni yake. Nchi ambayo miaka michache iliyopita ilitajwa kama mfano wa uchumi bora Afrika imekuwa ikikumbwa na kinachotajwa kama mzozo mbaya wa kiuchumi katika kipindi cha miaka mingi.

Waandamanaji zaidi ya 1,000 waliingia katika barabara za jiji kuu mwezi jana, wakitaka rais ajiuzulu na kulaani mikataba na IMF, ambayo walisema imefanya gharama ya maisha kuwa ya juu. Hii ni ishara ya yatakayotokea katika mataifa mengine ya Afrika yanayolemewa na madeni?



**Washington Gikunju**

**Nchi nyingi za Afrika, ziliathiriwa vibaya kwa kuwa zililazimika kuchukua mikopo ghali kujikinga na kununua chakula kwa raia wake wanaokumbwa na njaa. Mwezi huu tu, Ghana ilifanya kilichoonekana kutowezekana miaka michache iliyopita.**

Ni wakati utakaoamua. Kile ambacho hakina shaka, hata hivyo, ni kuwa itachukua juhudi zisizokuwa za kawaida kwa Kenya na nchi zingine zilizo na madeni Afrika kubadilisha hali inazozikumba kwa sasa.

Kama vile habari kuu ya wiki hii inavyoonyesha, itachukua zaidi ya kauli mbiu kuafikia miaka ya ufanisi wa uchumi chini ya utawala wa aliyekuwa rais Mwai Kibaki Mwandishi wa habari kuu, mwanauchumi mtajika Mbui Wagacha, anaonya dhidi ya sera ambazo zinaweza kusababisha serikali kuhudumu kwa kusudi zinazokinzana. Anasema kwamba Hazina ya Hasla, kwa mfano, ahadi iliyotolewa wakati wa kampeni ambayo kwa kiwango kikubwa ilichangia ushindi wa serikali ya Kenya Kwanza, hailandani na sera ya pesa ya Benki Kuu ya Kenya (CBK).

Huku CBK ikijaribu kukaza matumizi ya pesa ikilenga kuthibiti mufumuko, Hazina ya Hasla inataka kuweka pesa katika mfuko wa kila hasla, na kwa kufanya hivyo kuongeza presha ya mfumuko zaidi.

Juhudi za kutaka kufufua uchumi haraka anaonya, hazifai kurudisha mbinu za zamani za uchumi zinazohitaji kushirikisha sera za kifedha na za pesa. Wizara ya Fedha haiwezi kuhimiza kupunguzwa kwa bajeti huku ikiruhusu presha za kisiasa za kutumia pesa katika miradi ambayo wanasiasa wanatamani.

Vile vile, Benki Kuu ya Kenya, haiwezi kuhimiza sera ya kukaza pesa na ilhali inaruhusu utoaji wa mikopo kupitia simu za mikono, ambayo jukumu la kuthibiti ni lake. Hatimaye, ufufuzi wa uchumi utahitaji uzingatiaji wa dhati wa kanuni za kiuchumi, na uhuru kutoka kuingiliwa na wanasiasa.

Serikali ya Kenya Kwanza ni lazima ikubali kwamba ni rahisi kwa wanasiasa kuahidi muundo wa uchumi wa kuanzia raia wa tabaka la chini, lakini inafaa kuachia wataalamu wa uchumi kufanya kazi yao ili kutekeleza muundo huo.


*wgikunju@ke.nationmedia.com*

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

Darubini ya Wiki
Lilianzishwa na marehemu Hillary Boniface Ngweno
**Stephen Gitagama** Afisa Mkuu Mtendaji
**Joe Ageyo** Mkurugenzi wa Uhariri
**Washington Gikunju** Mhariri Msimamizi, Wikendi
**Mike Owuor** Mhariri Jumapili
**Allan Buluku** Mhariri wa Weekly Review
**Njoki Ndung'u** Mhariri wa Uchapishaji
**Andrew Anini** Msanifu Kurasa Mkuu
**Joan Pereruan** Mhariri wa Picha
**Humphrey Osoro, Alice Othieno** Wasanifu Kurasa

darubini

■ Jina la kitabu kipya limebakia siri




Mchoro wa jalada la riwaya ya *Asterix*. PICHA I HISANI YA CHARLES NDEGWA

# 'Asterix' yapata mwandishi mpya 2023

Kitabu maarufu cha ucheshi cha Kifaransa, Asterix kitazindua toleo la 40, huku mwandishi mpya akichaguliwa kuandika nakala ya mwaka ujao, mchapishaji wake alisema Jumanne.

Mwandishi wa riwaya Mfaransa, Fabcaro, maarufu kwa ucheshi wake wa kipekee, atakuwa mwandishi wa nne kuendeleza matukio ya shujaa Gaul, aliyesimama kidete dhidi ya Waroma.

Kama ilivyo desturi, toleo jipya litachapishwa mwaka usio wa kawaida, tarehe ya mwisho ya toleo hilo ikipangiwa Oktoba 26, 2023, alisema mchapishaji Albert Rene. Jina la kitabu kipya bado ni siri.

Asterix – mtetezi wa kijiji cha mwisho cha Gaulish kilichopinga utawala wa Kirumi - aliotewa mnamo 1959 na Rene Goscinny, aliyefariki 1977, na Albert Uderzo, aliyefariki 2020. Vitabu vyake vya ucheshi vimeuza mamilioni ya nakala kote duniani.

Kabla ya nakala za Asterix, hakukuwa na historia ya vitabu vya ucheshi kuwa na mwandishi wa hati. Fabcaro, 49, alisema ana furaha kuu kuchukua wajibu huo. "Nilikuwa shabiki mkubwa wa Asterix. Ilikuwa zawadi kubwa katika utoto wangu," akasema. "Nataka kuwa mwaminifu . . . kwa kinachofanya Asterix kuvutia. Mambo ya kipekee kama vile mbinu ya kurejelea kitu kwa wakati tofauti, kutumia maneno yanayomaanisha jambo zaidi ya moja . . . na hasa kuwa mwaminifu kwa wahusika."

Kama mwandishi mpya Fabcaro anafuata nyayo za waliomtangulia - Goscinny, Uderzo na Jean-Yves Ferri.

■ Wanahabari wazuiwa kusikiliza

# Kesi ya Suu Kyi hatua ya mwisho

Mahakama ya kijeshi itasikiza hoja za mwisho katika kesi iliyochukua miezi 18 ya Aung San Suu Kyi wa Myanmar wiki ijayo, duru zilisema Jumanne, kabla ya kufikia uamuzi wa mwisho dhidi ya mshindi huyo wa tuzo la Nobeli.

Suu Kyi amekuwa mfungwa tangu jeshi lilipoangusha serikali yake mnamo Februari 2021, na kumaliza kipindi kifupi cha demokrasia cha taifa hilo la Kusini Mashariki mwa Bara Asia.



Mshindi wa tuzo la Nobel Aung San Suu Kyi katika picha hii iliyopigwa Januari 17, 2020. PICHA I AFP

Amepatikana na hatia katika mashtaka 14 ya ufisadi, kumiliki vifaa vya mawasiliano vya polisi na kukiuka masharti ya Covid.

Mahakama itasikiza "hoja za mwisho" kutoka pande zote kuhusu mashtaka matano yaliyobakia ya ufisadi mnamo Desemba 26, amesema mtu anayefuatilia keshi hiyo. "Hukumu itatolewa baada ya hatua hiyo," akasema na kuongeza kuwa tarehe bado haijawekwa.

Suu Kyi, 77, alionekana mzima kiafya, akasema mtu huyo. Kila shtaka la ufisadi lina hukumu ya kifungo kisichozidi miaka 15 jela. Wanahabari wamezuiwa kusikiza kesi hiyo na mawakili wa Suu Kyi wamepigwa marufuku kuzungumza na vyombo vya habari.

Mnamo Juni, alihamishwa kutoka kifungo cha nyumbani na kupelekwa katika uwanja wa gereza ambako kesi yake inaendeshwa katika mahakama maalumu.

Jeshi lilidai kulikuwa na wizi wa kura wakati wa uchaguzi wa Novemba 2020 ambao chama cha Suu Kyi National League for Democracy kilishinda, ingawa waangalizi wa kimataifa walisema kwa kiwango kikubwa ulikuwa huru na wa haki.

Myanmar imekumbwa na michafuko tangu mapinduzi hayo huku watu zaidi ya 2,500 wakiuawa katika msako wa jeshi dhidi ya waasi.

■ Sh600m kwa wanaoishi maeneo kame

# Kukabili njaa msimu wa sherehe



Kamati ya Kitaifa ya Kukabiliana na Kiangazi inatazamiwa kuimarisha juhudi za kutoa msaada kwa Wakenya zaidi ya milioni nne katika maeneo kame yanayokabiliwa na njaa.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Afisa Mtendaji Mkuu wa Safaricom Peter Ndegwa, anasema wamechangisha zaidi ya Sh600 milioni kulisha wakazi wa maeneo kame msimu huu. Kamati hiyo inalenga kuchangisha Sh57.36 bilioni kufadhili mpango huo wa kukabiliana na kiangazi kati ya Januari na Oktoba 2023.

Wakenya wamehimizwa wachange pesa kupitia nambari ya Pay bill 880990 au KCB nambari ya akaunti 1305486137.

■ Gavana wa Meru atajua hatima yake wiki hii

# Seneti kuchunguza mashtaka ya Kawira



Gavana wa Meru anayepigwa vita Kawira Mwangaza wiki hii atajua iwapo pendekezo la madiwani wa Meru la kumtimua litaendelea mbele ya Seneti au litatupiliwa mbali.

Jumanne wiki iliyopita, maseneta walibuni kamati ya wanachama 11 kuchunguza mashtaka yaliyotolewa dhidi ya gavana huyo wa mara ya kwanza. Kamati hiyo ina siku 10 kuchunguza masuala saba ya madai dhidi ya Kawira na kuamua iwapo mashtaka hayo yamethibitishwa.

Kamati hiyo itahitajika kutoa ripoti kwa Seneti mnamo au kabla ya Desemba 30, 2022.

Gavana Mwangaza atahitajika kujitokeza kujibu mashtaka yaliyotolewa dhidi yake wiki hii.

*- Zimetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya kenya

■ JITIHADA ZA KUFUFUA NA KUDUMISHA UCHUMI THABITI

# UCHUMI: MIELEKEO TOFAUTI YATATIZA

**Ili kufufua uchumi wa Kenya, ni lazima mseto unaofaa wa sera ya kifedha upatikane. Lakini Benki Kuu na Hazina ya Kitaifa zimechukua mielekeo tofauti**

• Na Dkt Mbui Wagacha

Majuzi, nikiwa mwanajopo katika Mkutano wa 26 wa Benki ya Dunia kuhusu Hali ya Uchumi Kenya (KU), Desemba 8, 2022, mjadala ulizuka kuhusu mseto unaofaa kuhusu sera ya uchumi mkubwa (kuhusu fedha) unaohitajika kutia nguvu ufufuzi wa uchumi kuanzia na mabadiliko mafupi ya mwaka hadi mwaka katika uzalishaji, mapato na mahitaji.

Uchumi ungali unatatizwa na hali dhaifu ya kifedha na ukosefu wa sera na ushirikishi kuonyesha jinsi mseto wa sera utatekelezwa kuufufua. Utata huu mkubwa unamaanisha kuwa pande zote mbili zinashirikiana kulinda kuzorota kwa miaka ya hivi majuzi, kufutwa kwa wafanyakazi na mabadiliko ya kifedha.

Kwa miongo miwili baada ya utawala wa Moi, juhudi za uongozi wa Kenya kuafikia mseto huu na kufufua uchumi katika muda mfupi, wa kati na mrefu zinaonyesha ufanisi na kufeli.

Viongozi wenye kusudi huchukua hatua zaidi za kuepuka kuporomoka kwa uchumi, wakitumia sera kuu mseto na kuvumilia hata mijadala mikali ya umma na kuchukua hata hatua zizisokuwa za kawaida, ikibidi. Matokeo yanaweza kuokoa uchumi kama ilivyotokea kwa Fed Bernanke nchini Amerika wakati wa mzozo wa kifedha wa 2008-09. Uokoaji wa benki kutumia pesa za mlipa ushuru ulikataliwa. Iliibuka kuwa hatua ya ujasiri ambayo Amerika ilihitaji kuokoa uchumi; ulipaji wa riba ulifanywa baada ya ufufuzi. Kinyume na hilo, nchi za bara Ulaya zilipambana na shida kama hii.

Katika Kenya, mwathiriwa mkubwa wa utata wa sera za serikali iliyoondoka ya Jubilee na athari za janga la Covid-19 na vita vya Urusi/Ukraine ni kilimo, ambacho Wakenya wengi hushiriki na kuchangia asilimia 20 ya pato la nchi (GDP).

Kudorora kwake kwa asilimia 1.5 nusu ya kwanza ya mwaka wa 2022, kulichangia kupungua kwa asilimia 0.3 ya GDP. Matokeo yanaonyesha kuwa kuongezeka kwa umaskini na ukosefu wa usawa, ukosefu mkubwa wa ajira na mapato ya chini ambayo yanaweza kuongezwa kwa uzalishaji wa juu, viwanda vya kutengeneza bidhaa za kilimo, unyunyuzaji na kadhalika.

Takwimu zinaonyesha kwa jumula mapato yanaendelea kupungua. Wengi wa watu 2.9 milioni pekee walioajiriwa katika sekta rasmi ya Kenya wanapata mishahara midogo, huku 358,833 pekee au asilimia 15 wakipata zaidi ya Sh100,000 kwa mwezi. Wafanyakazi wengine 1.18 milioni au asilimia 40 wanapata chini ya Sh50,000 kwa mwezi na wapatao 51,770 wanapata chini ya kiwango cha mishahara cha kitaifa cha Sh20,123. Kinyume na hilo, Wakenya 3,362 walikuwa mabilionea kufikia mwisho wa 2021, na inakadiriwa watafika 4,274 kufikia 2026.



Prof Njuguna Ndung'u | DIANA NGILA



Dkt Patrick Njoroge | DIANA NGILA

Ujumbe wa maafisa wakuu wa Wizara ya Fedha katika mkutano wa Benki ya Dunia ulikubali suluhu ya Benki ya Dunia kuwa mojawapo ya kukabiliana na athari za hivi majuzi ni kuweka kilimo mbele na katika mseto wa sera, kupunguza matumizi kunaweza kuimarisha fedha huku mikopo ikitolewa kwa sekta ya kibinafsi kuwezesha ukuaji. Mseto huu unaweza kufikiwa kupitia mikopo nafuu katika mfumo wa kifedha na kupunguza matumizi ya serikali.

Kwa bahati mbaya, Benki Kuu ya Kenya, kama iliyo na jukumu la Kikatiba, kwa sasa imekaza viwango vya riba ikitaja hali duniani, badala ya ushirikishi wa upande wa kifedha.


Inakosa msimamo, ikichochea matumizi au kutangaza kupunguza matumizi, wakati mwingine ikikanganya au hata kubadilisha hatua inazotangaza.

Rais hajashauriwa ipaswavyo kuhusu hali zote mbili. Kwa mfano, CBK inajiingiza katika udhibiti kuzuia kunyemelewa kwa sera ya kifedha na wakopeshaji wa dijitali kutoka mataifa tajiri wanaotumia uwezo wa simu za mkono kubadilisha sehemu ya jamii yetu kama maabara ya kujitajirisha.

Hiyo ni pamoja na makosa ya utawala wa Jubilee ambao ulirithisha Kenya hali mbaya ya uchumi. Serikali ya Kenya Kwanza itanufaika kwa kusoma mazuri na mabaya ya juhudi za miongo miwili za kufufua uchumi na uthabiti. Moja ni mpito wa utawala wa Moi hadi wa Kibaki, ambao waliofanikisha sera kubwa mseto, Mundell, Tinburgen, Tobin, na Okun wanaweza kuupongeza.

Jedwali la kwanza linaonyesha ukuaji wa enzi ambayo ilifufua GDP kutoka kuporomoka kulikorithiwa kutoka Moi hadi asilimia 8.4 kufikia 2010 kutoka asilimia 0.5 mnamo 2002.

Endelea Uk 6







Nation Media Group "ePaper Copy"

# Makusudio tofauti

Kutoka Uk 5

Kiwango cha ukuaji wa GDP cha asilimia 0.2 pekee mnamo 2008 kinaonyesha jinsi Kibaki alitumia mseto wa sera kuu baada ya mzozo wa kifedha wa 2008-09 ambao ulifuata ghasia za kikabila Kenya.

Ukuaji uliimarika kufikia asilimia 8.4 mnamo 2010. Je, hii iliafikiwa vipi? Baada ya 2002, tangazo la kupunguza ukopaji kutoka CBK lilipunguza mikopo kwa serikali, na kukopesha sekta ya kibinafsi kwa ongezeko la mwaka kwa mwaka, mahitaji na mapato. Ukuaji ulifikia asilimia 6.9 kufikia 2007. Kiwango cha deni kwa GDP cha asilimia 60 kilipunguzwa hadi asilimia 40 kufikia 2008 kupitia uwekezaji, kuongezeka kwa nafasi za ajira, ukuaji wa mapato katika KRA na ulipaji wa madeni.

Jedwali la kwanza pia linaonyesha jinsi serikali iliyoondoka ya Jubilee ilifanya vibaya ikilinganishwa na viwango alivyoweka Kibaki kuanzia 2013. Utendaji wa 2021-2022 (nusu ya kwanza) unaonyesha ufufuzi kutoka chini ya sufuri wa ukuaji wa GDP mwaka wa 2020.

Mistari inaonyesha kuwa ni Kibaki aliyekaribia malengo ya Ruwaza ya 2030 ya ufufuzi wa GDP wa asilimia 10 ikilinganishwa na tawala za Moi na Jubilee ambazo ziliacha uchumi katika hali mbaya. Vilevile, jedwali la pili linaonyesha utawala wa Kibaki ulitumia usimamizi wa uchumi kupunguza madeni na kuimarisha imani ya biashara huku utawala wa Jubilee ukisukumia Kenya madeni baada ya 2013.

Ni nini kinaweza kuimarishwa katika mbinu ya Kenya Kwanza? Mafunzo ya sera mseto yanapendekeza ufufuzi (uwekezaji, faida, ajira) unaweza kuanza na sera legevu ya pesa (kupeleka mikopo kwa sekta ya kibinafsi kupitia benki za kifedha na uwezeshaji wa huduma za simu za mikono) na kukaza matumizi (kupunguza matumizi ya serikali); au inaweza kuafikiwa na kulegeza fedha (kuongeza matumizi) na kukaza sera ya pesa (viwango vya juu vya riba). Maswali yanakumba Kenya Kwanza kuhusu ukosefu wa uadilifu ambapo sera za kifedha ni tofauti, hata ndani ya kila sehemu.

Hali ya kifedha bado inakumbwa na uzembe na mkanganyiko wa ushuru, msamaha usio na mantiki wa ushuru, upuuzaji wa makubaliano ya ushuru uliotambuliwa na IMF kwa wawekezaji ambao unakosa kufaidi uchumi na ongezeko la ukuaji katika uwekezaji, nafasi za ajira na bei nafuu kwa bidhaa za matumizi.

Baada ya kujitolea mapema kupunguza matumizi kwa Sh300 bilioni, matumizi na ukopaji wa wazi unakinzana na presha za kisiasa za matumizi, hasa na viongozi wa serikali kuhusu miradi wanayopenda. Hali hii ya inawafanya wakose kuona hatari iliyopo, huku tukikodolea macho hatari mbaya zaidi ya Kenya kutumbukia kwenye shimo la kiuchumi.

Kwa upande mwingine, hali dhaifu ya pesa inajaribu kukazwa na benki kuu duniani, huku ikizimwa na wadau wa dijitali (ikiwemo Hazina ya Mahasla) inayofanya sera kuwa dhaifu zaidi. Ukweli kuwa mikopo ya sekta ya kibinafsi iliongezeka kwa zaidi ya asilimia kumi tangu Machi 2022 hadi asilimia 12.5, unamaanisha ukazaji hauna faida.

Hali zingine zinazoweza kutatuliwa iwapo udhibiti wa Benki Kuu unaweza kutiwa nguvu na kushirikishwa na Wizara ya Fedha ni pamoja na kudhibiti mfumko.

Hazina ya Kitaifa imechukua hatua za kushangasha bila majadiliano ya kimsingi. Inashughulikia presha za madeni bila suluhu kuhusu pesa. Kufikia sasa tumesikia kuhusu mikopo mipya isiyo na riba ya juu (inapatikana kweli?) na kuilipa kwa ukopaji wa ndani ya nchi.

Suluhu ya kwanza inapuuza vigezo muhimu, mfumko na viwango vya ubadilishaji ambavyo vinaweza kuwa na manufaa baada ya mikopo na madeni mengine.


Kuzozana na Fitch kunaweza kuharibia mtu aliye Kenya soko la kifedha. Njia ngumu na ya pekee ya ufufuzi ni kujenga sekta za uchumi chini ya sera mseto.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

---

■ DALILI ZA KIGOGO ANAYEIBUKA

## Riggy G anashughulika kujijenga kuwa msemaji wa Mlima Kenya




● Na JOHN KAMAU

Katika siasa, Geoffrey Rigathi Gachagua, 57, ni mtu mwoga. Kwa siku100 zilizopita, mwanasiasa huyo aliyezaliwa Nyeri amekuwa na kazi nyingi akijijenga na kubuni mikakati ya kuimarisha uongozi wake katika eneo la watu wengi la Mlima Kenya, linalojumuisha kura za Wakikuyu, Wameru na Waembu.

Bw Gachagua yuko karibu sana na urais - lakini itategemea jinsi ataendesha siasa zake za kitaifa na za Mlima Kenya. Akilinganishwa na manaibu rais 11 waliohudumu Kenya (walioitwa Makamu Rais), Gachagua amejitokeza kuwa mwanasiasa anayependa umaarufu na mwenye nguvu kama Jaramogi Oginga Odinga miaka ya 1960 na Dkt Josephat Njuguna Karanja katika miaka ya 1980, kabla ya wawili hao kutemwa. Uchangamfu wake pia ni sawa na wa Dkt Ruto, labda kutokana na kuwa walikuwa wanaharakati wa Kanu wakiwa wanafunzi wa chuo kikuu.

Katika siasa za kitaifa, Bw Gachagua ni mwanasiasa lim-

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

## kurunzi ya kenya

bukeni - lakini hawezi kulinganishwa na Dkt Josephat Njuguna Karanja, Moi alipomteua makamu rais mnamo Machi 24 1988, kuchukua nafasi ya Mwai Kibaki waliyekuwa wametofautiana. Huku Bw Gachagua akiwa amehudumu kama mbunge kwa muhula mmoja akiwakilisha eneobunge la Mathira, Dkt Karanja alikuwa amehudumu kwa miezi 14 kama mbunge wa Mathare kabla ya kuteuliwa Makamu Rais.

Jinsi tu Bw Gachagua alivyo leo, Dkt Karanja alionekana mtu aliyekuwa na haraka ya kujiimarisha – jambo lililokasirisha washirika wa karibu wa Moi. Kwa kujaribu kujenga himaya yake mpya ya mamlaka, Dkt Karanja alitimuliwa baada ya kuwa ofisini kwa siku 103, Moi alipotumia wanasiasa wawili wa eneo la Kati, Kuria Kanyingi na David Mwenje kumzima. Dkt Karanja kwanza alilaumiwa kwa kuwataka viongozi 'wampigie magoti' kisha akalaumiwa kwa kujifanya 'kaimu' rais, Moi alipokuwa ng'ambo. Hatimaye, Bunge lilipitisha kura ya kutokuwa na imani naye.

Kwa sababu ya ngome yake mpya, huenda ikawa vigumu kumpuuza Bw Gachagua katika siasa za Kenya. Baada ya eneo la Mlima Kenya kushiriki uchaguzi mkuu uliopita bila msemaji au kiongozi, hali inayoibuka ni kuwa Bw Gachagua anapigania nafasi hiyo.

Baada ya aliyekuwa Rais Uhuru Kenyatta kuondoka, siasa za Mlima Kenya ziliachwa bila kiongozi. Kushindwa kwa mgombeaji wake, Raila Odinga, kuliacha eneo hilo likitafuta mtu mwingine. Rais Kenyatta hakuchagua mrithi wake ndani ya eneo la Mlima Kenya, akitarajia kuwa angeendelea kuamua watakaokuwa viongozi wa eneo hilo. Lakini, pia, hatua ya Rais Ruto ya kumuondoa kutoka siasa za humu nchini ilimaanisha hana wakati wa kuongoza wanasiasa wa Mlima Kenya.

Kwa siku 100 zilizopita, Rais mstaafu Kenyatta amekuwa akihusika na juhudi za kimataifa za kuleta utulivu katika Jamhuri ya Demokrasia ya Congo na kutatua mzozo wa Ethiopia. Kutokana na shughuli hizo nyingi - na akiwa na wajibu wa kiongozi mashuhuri - Rais Kenyatta ameamua kujiondoa kama mwanachama wa Muungano wa Azimio One Kenya, hatua ambayo inamuondoa katika kusimamia siasa za eneo la Mlima Kenya.


Kufuatia kuondoka kwa Uhuru katika siasa za humu nchini hadi za kimataifa, Bw Gachagua ndiye kiongozi wa kisiasa mwenye nguvu katika eneo hilo.

Kwa hisani ya Katiba ya 2010, wadhifa wa Bw Gachagua umelindwa na hawezi kutimuliwa alivyofanyiwa Bw Kibaki baada ya kutengwa kwa muda mrefu au kwa njia iliyotumiwa kumuondoa Dkt Karanja. Hivyo basi, hata kama anaonyesha azma ya kung'aa kuliko Dkt Ruto, itakuwa vigumu kumuondoa mamlakani chini ya Kifungu cha 150 - ikizingatiwa kuwa wabunge wa UDA kutoka Mlima Kenya ni wengi na kwa kuwa rais anamhitaji kushinda muhula wa pili.

Kwa sasa, Bw Gachagua anajua hakuwa maarufu ndani ya chama cha UDA kuteuliwa naibu rais. Na hii inaeleza ni kwa nini katika siku 100 zilizopita, ametumia muda wake akitafuta maridhiano - na kuweka vizingiti - kuimarisha ushawishi wake katika eneo hilo.

Wakosoaji wake wanasema hali yake ya kukosa ujuzi wa kuendesha serikali inaonekana katika matamshi yake ya sera na maamuzi yasiyo rasmi ilivyokuwa katika utawala wa Kanu.

Kama atafaulu kuungwa mkono na wanasiasa wa Mlima Kenya na matajiri waliomuunga mkono Raila katika uchaguzi mkuu uliopita, Bw Gachagua atakuwa mtu mwenye nguvu.



Rais William Ruto.
PICHA I MAKTABA

Hasa, hatakuwa mtu wa kupuuza katika siasa za eneo lake. Lakini hili litawezekana kama atajijenga katika Mlima Kenya badala ya chama cha UDA. Hata miongoni mwa wafuasi wa UDA, gumzo katika eneo la Mlima Kenya ni kuwa eneo hilo linahitaji chama chake cha kisiasa.

Wakati wa kampeni, Rais William Ruto aliambia mikutano kadhaa ya kisiasa alikuwa "Msemaji mpya wa Mlima Kenya" na kukasirisha washirika wa Uhuru.

Bw Gachagua anajua Dkt Ruto alichaguliwa kwa sababu ya umaarufu wake eneo hilo. Lakini uzalendo wa kikabila unapochukua nafasi ya kwanza katika eneo la Mlima Kenya, inaonekana Bw Gachagua atakuwa katika hali aliyokuwa Musalia Mudavadi katika Magharibi mwa Kenya na Moses Wetangula wa Ford Kenya.

Wiki iliyopita akiwa Nyeri, Gavana wa eneo hilo Mutahi Kahiga, alitangaza kuwa Bw Gachagua ndiye msemaji mpya wa Mlima Kenya - na kuwa ndiye anfayefaa kuongoza siasa na wanasiasa wote wa eneo hilo.

Pia, alimshambulia aliyekuwa gavana wa Murang'a, Mwangi wa Iria, kwa kuongoza upinzani dhidi ya Bw Gachagua. Naibu Rais anasema ameweka makataa ya Desemba 31 kwa wapinzani eneo la Mlima Kenya walio katika Azimio wamuunge mkono na Rais Ruto. Hata hivyo, matukio ya hivi majuzi yanaonyesha amekuwa akifanya maridhiano na kuzungumza na upinzani.

Kuchaguliwa kwa aliyekuwa Mbunge wa Kieni Kanini Kega, mgombeaji wa Jubilee, katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA) kupitia juhudi za Bw Gachagua, kulikuwa ishara ya kwanza ya jinsi anataka kuendesha siasa zake.

Hivi majuzi, Bw Gachagua amekuwa akitoa maagizo katika mikutano yake hata kuhusu kazi za mawaziri. Sauti yake mpya ya kuamuru na ujasiri ni dalili za mtu anayedhibiti siasa zake. Pia ameibuka kuwa mtetetezi wa biashara za Mlima Kenya. Kwenye mkutano katika ngome yake ya Nyeri majuzi, Naibu Rais alimuonya Gavana wa Nairobi, Johnson Sakaja, dhidi ya kuingilia matatu jijini Nairobi, akisema: "Ni sisi tulikuchagua." Matamshi yake yalifuatia malalamishi ya wenye matatu kutoka Mlima Kenya.

Ingawa magavana hawafai kupokea amri kutoka kwa serikali ya kitaifa, Bw Gachagua yuko tayari kuvuka mpaka huo. Huenda uwezo huo umetokana na majukumu yake mapya. Baada kuapishwa kuwa Rais, Dkt Ruto alitangaza kuwa kama sehemu ya majukumu ya naibu rais, Bw Gachagua atashirikisha "uhusiano kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti." Jinsi Naibu Rais anatafsiri majukumu hayo itaamua uhusiano wake wa kikazi kati ya serikali ya kitaifa na serikali za kaunti.

Rais Ruto, bila kujua, alimruhusu Bw Gachagua kuunda himaya mpya ya mamlaka kwa kumpa majukumu maalumu ya kitaifa.

Akiwa Naibu Rais, Dkt Ruto alikuwa na wakati mgumu kwa kuwa Rais Kenyatta hakumtengea jukumu lolote maalumu. Tofauti na makamu rais wa zamani chini ya Jomo Kenyatta, Moi na Mwai Kibaki, waliopewa nyadhifa za uwaziri, Dkt Ruto alitazama huku mawaziri wakipewa kazi ambazo Naibu Rais angefanya.

Ingawa Katiba Mpya ya 2010 iliacha Naibu Rais bila jukumu muhimu isipokuwa kuwa msaidizi mkuu wa Rais, uamuzi wa Dkt Ruto wa kumpa majukumu naibu wake unajiri na hatari za kisiasa. Hawezi kumpokonya majukumu hayo, bila kutofautiana kisiasa.

Jaramogi alipopewa majukumu kama hayo, alikosana na watu kadhaa kwa kutoa maagizo ya kutimuliwa nchini kwa wageni akijaribu kusaidia Jomo Kenyatta kuongoza nchi baada ya uhuru. Lakini, alivyoandika baadaye, juhudi zake zilichukuliwa kama za kupindua serikali ya Kenyatta.

Baadhi ya majukumu muhimu yaliondolewa kutoka Wizara ya Mashauri ya Ndani ili kupunguza makali yake. Hatimaye, baada ya siku 488 akiwa Makamu Rais, Oginga alikata tamaa na akajiuzulu Aprili 14, 1966, kuunda chama cha Kenya People's Union.

Katika wadhifa wake mpya, Bw Gachagua anasimamia kamati za Baraza la Mawaziri na utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri katika Wizara na Idara zote. Pia anasimamia Baraza la Bajeti na Uchumi la viwango vyote vya serikali (IBEC), jukumu la pekee la Kikatiba la Naibu Rais.

Zaidi, anashirikisha tume za kikatiba na afisi huru katika masuala yanayohitaji kuhusika kwa serikali, ikiwemo bajeti, uundaji wa sera na utekelezaji wa mapendekezo yake.

***jkamau@ke.nationmedia.com***

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni




■ Wanawake hutarajiwa kuvaa kiadabu na kiheshima, lakini wanaume husimamia sheria hiyo

# Kauli ya Duale kuhusu Hijabu ni kitisho



KWENDO
**OPANGA**

Waziri wa Ulinzi, Aden Duale, huwa haoni kashfa kama ganda telezi la ndizi. Hasa, kama ingekuwa, kisha aione upande mwingine wa barabara, angevuka na kuikanyaga ili eteleze.

Bila kuchokozwa, Duale wiki iliyopita aliambia wanawake Kenya wasiotaka kuvaa hijabu wafunge virago na kutokomea mbali kwa sababu "Wanawake Waislamu watavaa hijabu" katika maeneo ya umma.

Kuvaa hijabu, alidai Duale, ni utamaduni wa Kiislamu. Lakini kwa kuwataka wasiotaka kuvaa watafute uraia au makao mengine, waziri alimaanisha hakuna namna nyingine katika suala hili. Haliwezi kujadiliwa.

Bila shaka Duale anajichukulia kuwa mlinzi au msimamizi wa adabu na nidhamu ya wanawake Waislamu. Nasema nidhamu kwa sababu hiyo hasa ndiyo maana ya hijabu. Hijabu imetajwa mara nane katika Koran, na inahusu Waislamu, wanawake kwa wanaume, kuvalia kiheshima, kuwa na nidhamu, kufunika sehemu zao nyeti na kuepuka majaribu ya kingono. Lakini ni sharti isemwe, sio wote wanaovalia hijabu wanaofanya hivyo kwa sababu hizo. Ni vazi lenye utata.

Moja, kama ambavyo televisheni ya World Is One (WION) imeripoti mara kadhaa, baadhi ya wanawake huvaa hijabu kwa sababu ya dini, wengine kwa sababu ya utamaduni wao, baadhi kwa sababu ndivyo familia inavyofanya, wengine huvaa kama kitambulisho. Baadhi huvaa kila wakati ilhali wengine huvaa wakienda kusali. Vazi hili la hijabu linalazimishwa kwa baadhi ilhali wengi hulivaa kwa hiari.

Pili, baadhi ya watu Ulaya, zikiwemo serikali, wasema Waislamu wanaotaka kufanya mataifa ya Ulaya kuwa makazi yao ni lazima wafuate mtindo wa nchi wanazohamia, na kuvaa hijabu huwatofautisha na wengine, humaanisha wao ni tofauti na hawataki kujumuishwa katika tamaduni mpya. Hasa, kwa sababu za kiusalama, nchi kadhaa za Ulaya zimepiga marufuku kabisa hijabu.

Tatu, baadhi wanasema hijabu si vazi la lazima kwa sababu hilo si agizo katika Koran jinsi ilivyo katika nguzo tano kuu za Uislamu, ambazo ni kukariri imani (shahada), sala (salat), zaka (zakat), mfungo (sawm) na kwenda kuhiji (hajj). Hivyo basi, hoja hiyo inasema kuvaa hijabu si lazima bali ni hiari.

Nne, vipande vya nguo vinavyotumika kwa sababu zilizotajwa awali vinatofautiana. Khimar hufunika kichwa, shingo na mabega. Burqa hufunika mwili mzima. Niqab hufunika uso tu. Chador hufunika mwili mzima isipokuwa macho. Hijabu hufunika kichwa na shingo. Lakini ni nani wanaovaa aina zote hizi za mavazi ya kujisitiri kwa sababu ya adabu na heshima? Ni wanawake. Ni nani wanaosimamia sheria hii? Wanaume.

Tano, wanaume, hasa walio mamlakani, hufanya suala hili kuwa gumu. Tafakari. Mnamo 1936, Reza Shah Pahlavi, alipiga marufuku vitambaa vyote vya kufunika uso. Umma ulivamia wanawake waliovaa vitambaa na kuvirarua. Mnamo 1981, wapiganaji wa Ayatollah waliotwaa mamlaka Tehran 1979, walitoa amri iliyotangaza hijabu kuwa lazima. Wanawake waliopatikana bila hijabu walikamatwa na kuzuiliwa.

Nchini Uturuki, baadhi ya simulizi zinasema Mustafa Ataturk alipiga marufuku vitambaa vya kichwani katika sehemu za umma alipozindua marekebisho ya katiba mnamo 1924. Wengine husema hakukataa bali alipendekeza tu. Vyovyote vile, mnamo 2013 aliyekuwa waziri mkuu enzi hizo, ambaye sasa ni Rais, Tayyip Erdogan, aliondoa marufuku hiyo iliyodumu kwa miaka 89.

Mwisho, Duale alionekana kumaanisha kuwa vyombo vya habari vilitaka kumtishia kwa sababu vilimkosoa kwa kuamuru wanawake wavae hijabu la sivyo waondoke nchini. Hapana, ni Duale aliyetishia wanawake wa Kenya.

*kwendo58@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Mary Wangari*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

maoni

Lazima Rais abuni idara mahsusi ili kulainisha mkondo wa mawasiliano katika serikali

# Viongozi wanatuchafulia hewa kwa matamshi yao



MACHARIA GAITHO

Tunaona mara nyingine jinsi siku 100 baada ya kuchukua uongozi, kinajitokeza sana katika serikali changa ya Rais William Ruto ni utoaji jumbe zinazokinzana.

Ni wazi kuwa baadhi ya mawaziri wanapofungua midomo yao, kinachotoka ni jumbe kinzani zinazoonyesha hali ya mkanganyiko, utovu wa nidhamu na uchafu iliyo serikalini.

Makosa ya kimatamshi yamekuwa hali ya kawaida. Mwishowe, huwa tu hayamwaibishi waziri anayehusika, bali yanaonyesha serikali mpya kama iliyochanganyikiwa badala ya iliyolainika.

Kila wakati kiongozi anapotoa tamko lisilofaa, lazima likanushwe mara moja huku vyombo vya habari vikitishiwa vinaporipoti. Ishara iliyopo ni kuwa kuna tatizo kubwa serikalini, ambapo mkono wa kulia haujui unachofanya mkono wa kushoto.

Katika hali hiyo, ni vigumu kujua nguzo kuu za sera ya serikali ya Kenya Kwanza, kando na mazoea ya kuilaumu serikali ya Rais Mstaafu Uhuru Kenyatta na Naibu Rais William Ruto kwa kukosa kutimiza ahadi zake.

Rais Ruto amefanya vyema kuwapa mawaziri uhuru wa kuendesha majukumu yao bila kuwa na mazoea ya kuomba ushauri kila mara kutoka kwa ofisi yake huku wakielezea kwa kina sera na mipango ya serikali.

Kama matokeo ya uamuzi huo hayajawa ya kuridhisha, basi lazima Rais achukue hatua. Ni lazima walio na mazoea ya kutoa matamshi ya kukanganya waambiwe wakome kuhutubu mbele ya umma, la sivyo wawe wakisoma hotuba zilizoandikwa.

Lazima Rais abuni idara thabiti ya kusimamia mawasiliano ya serikali ambayo itahakikisha kuwepo kwa utaratibu mzuri wa mawasiliano katika serikali nzima.

Anapaswa kuanza nyumbani kwake, ambako mwanawe amezua hisia mseto kwa kudai anashikilia 'Ofisi ya Bintiye Rais' inagwa hakuna ofisi kama hiyo katika katiba. Yeye si jamaa wa kwanza wa familia zinazotawala kuchanganywa na mamlaka.

Hata hivyo, mwanasiasa mwenye uzoefu mkubwa anayeshikilia nafasi muhimu kama Waziri wa Ulinzi anapotoa taarifa zinazoweza kuzua taharuki za kidini ni lazima akabiliwe vikali.

Bw Aden Duale si mgeni katika mamlaka. Alishikilia nyadhifa muhimu za uongozi katika vipindi vyote viwili vya serikali ya Jubilee, ambapo kwa sasa, anafaa kujua tofauti kati ya matamshi ambayo mwanasiasa wa kawaida anafaa kutoa na yanayofaa kutoka kwa kiongozi anayezungumza kwa niaba ya serikali.


Katika hali ya kawaida, matamshi yake kuhusu haki ya wanawake Waislamu kuvaa hijabu yanafaa kukaribishwa katika nchi yenye utamaduni wa kuzingatia uhuru wa kidini na matabaka tofauti. Kisichokubalika ni pale kauli ya Waziri wa Ulinzi inapoonekana kujaa vitisho.

Kunaweza kuwa na nafasi ya majadiliano kuhusu iwapo alisema wanaopinga uvaaji hijabu wanafaa kuondoka Kenya na kutafuta hifadhi katika nchi nyingine, au wanawake Waislamu ambao hawavai vazi hilo wanafaa kuondoka nchini pia.

Kisingizio eti alikuwa akihutubia jamii fulani hakina msingi wowote, kwa sababu alikosolewa kote nchini wala si katika eneo moja tu.

Duale anafaa kukumbuka kuwa yeye ni Waziri wa Ulinzi wa Jamhuri ya Kenya, wala si wa Kaunti ya Garissa, jamii ya Wasomali au Waislamu.

Iwapo anataka kujijenga kama kiongozi wa kijamii, ana kila haki kujiuzulu kama Waziri na kurudi katika siasa za Garissa au atafute nafasi ya uongozi katika Baraza la Kitaifa la Waislamu Kenya au taasisi nyingine kama hizo.



Waziri wa Ulinzi Aden Duale akihutubia mkutano katika Sir Ali Muslim Club, Parkroad, Nairobi, mnamo Desemba 20.
PICHA ISILA KIPLAGAT

Anafaa pia kudhibitiwa iwapo amelewa na mamlaka. Kwa miaka mingi nchini, Waziri wa Ulinzi amekuwa tu kama mwakilishi. Wakuu wa kijeshi huripoti moja kwa moja kwa rais, kwani ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Kenya na Waziri Mtendakazi wa Ulinzi.

Duale amezua mjadala usiofaa ambao katika siku zijazo, utaashiria kiwango cha mamlaka yake, kwa mfano, hawezi kutoa maagizo kuhusu utaratibu fulani wa mavazi katika jeshi.

Kwa vyovyote vile, hakuwa na sababu yoyote muhimu ya kutoa vitisho kuhusu uvaaji hijabu kwa kuwa hakukuwa na dalili zozote zilizoonyesha mfumo wa mavazi wa jamii ya Kiislamu ulikuwa umetishiwa.

Kama kuna wakati kutakuwa na haja ya kubuniwa kwa sera ya mavazi ya Kiislamu, Wakorino, Sikh na madhehebu mengine katika jeshi, polisi ama vikosi vingine vya usalama, hilo litaangaliwa vizuri kupitia taratibu zilizopo wala si kupitia matamshi ya kisiasa.

Duale si kiongozi pekee mwenye mazoea ya kutoa matamshi ya kiholela. Anaonekana kumwiga Naibu Rais Rigathi Gachagua, ambaye tayari anajulikana kwa mtindo huo.

Gachagua anaonekana kutolinda matamshi yake kama Naibu Rais, kwani amezidisha mazoea ya kutoa matamshi na vitendo hatari vinavyoashiria pengo kubwa lililopo katika mfumo wa mawasiliano serikalini.

Mtindo wake wa kutoa maagizo yenye uzito kwenye mikutano ya barabarani unaashiria kurudi kwa mfumo wa utawala wa enzi za Moi.

Tumemuona akipokea mabunda ya noti katika hafla za umma, na sasa akikiuka taratibu za kuajiri watu za serikali kwa kuagiza watu wanaomfikia katika mikutano ya umma kuajiriwa mara moja.

Gachagua ni mtu mwingine anayeonekana kufikiri kuwa ofisi anayoshikilia inamlinda dhidi ya kutokabiliwa kisheria kwa kukiuka taratibu za utumishi wa umma. Hivi karibuni au baadaye atajua kuwa anapewa kamba ndefu sana kujinyonga yeye mwenyewe.

*gaithomail@gmail.com*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media


# habari kwa picha



Shabiki wa Argentina aliye juu ya mlingoti ashangilia wachezaji wa timu hiyo wakiwa juu ya basi katika jimbo la Buenos Aires mnamo Desemba 20, 2022 waliporudi nyumbani baada ya kushinda Kombe la Dunia la Qatar 2022. PICHA | AFP



Magari yakipita karibu na mapambo ya kuadhimisha Krismasi na Mwaka Mpya jinni Tbilisi, Georgia, mnamo Desemba 20, 2022. PICHA | AFP



Picha hii iliyopigwa kutoka angani mnamo Desemba 21, 2022 inaonyesha waendeshaji magari wakisafiri katika eneo lililofurika la Matangkuli, Indonesia. PICHA | AFP



Mtunzaji wa Ndovu, Kiapi Lakupanai, akicheza na ndama wawili katika Hifadhi ya Wanyamapori ya Namunyak, Samburu, Kenya mnamo Oktoba 12, 2022. Ndama mayatima na wengine walioachwa wameongezeka kutokana na ukame wa sasa. PICHA | AFP



Vazi la Kiarabu (bisht) rangi nyeusi na dhahabu likishonwa katika duka la Al Salim, jijini Doha, Desemba 20. Vazi hilo limefanywa maarufu na mchezaji wa Argentina, Lionel Messi. PICHA | AFP



Maelfu ya ndege aina ya Pengwini waliopigwa picha Desemba 21, katika Kisiwa cha Desolation, kusini mwa Bahari ya Hindi. PICHA | AFP



Wanariadha wakitumbuiza ufuoni kabla ya Michezo ya 10 ya Mombasa ya Kuwania Ubingwa wa 2022 wa Karate ya Tong-IL Moo-Doo wikendi iliyopita. PICHA | AFP

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya afrika

MABADILIKO YA TABIANCHI DUNIANI

# MATUKIO MFULULIZO YA LA NIÑA YASABABISHA MAAFA MKUBWA




**Wanachama wa Huduma za Polisi Afrika Kusini wakiondoa mwili wa mtu aliyetoweka kufuatia mvua ya mafuriko katika eneo la Soweto, Afrika Kusini, mnamo Desemba 11.** PICHA I AFP

## Afrika Kusini imekumbwa na msururu wa visa hatari vya mabadiliko ya hali ya hewa ambavyo vimeacha maelfu ya watu wamekufa, mali kuharibiwa na miundomsingi kuporomoka

• Na Chris Erasmus

Maelfu ya raia wa Afrika Kusini wamelazimika kutoroka makwao, na vifo kadhaa vimetokea, mali na shughuli za maisha kuharibiwa baada ya nchi hiyo kukumbwa na hali 'nadra' ya hewa ambayo imekuwa ikitokea, na ambayo, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi ulimwenguni, imekuwa janga linalojirudia.

Sehemu za Afrika Kusini, ikiwemo Johannesburg na viunga vyake, zimekumbwa na visa vinavyojirudia vya matukio ya mvua kubwa siku za hivi majuzi, huku matukio zaidi yakitarajiwa. Hali hii, wanasema wataalamu wa hali ya anga, si ya kawaida, lakini imeendelea kutokea na wanasayansi wana hakika ni sehemu ya mabadiliko ya tabia nchi, linavyosema Shirika la Kimataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabia nchi (IPCC).

Hali hii inazidishwa na ukweli kuwa 2022 ni mwaka wa tatu mfululizo wa hali ya 'La Niña', kuonyesha mabadiliko katika mawimbi ya maji ya Bahari Pacific.

La Niña (jina la Kihispania linalomaanisha "msichana") inamaanisha hali ya hewa yenye mvua na viwango vya juu vya joto majira ya joto ya sehemu ya kusini ya ulimwengu, huku El Nino (mvulana) ikimaanisha kinyume chake.

Hali hizi mbili ni vipindi vya baridi na joto vya hali ya bahari inayoitwa El Nino -Southern Oscillation (ENSO). Hali hii inatokea kila miaka miwili hadi saba na inasababisha mabadiliko yanayotarajiwa katika viwango vya joto na mvua.

La Niña ni kipindi cha baridi cha ENSO, lakini hii haimaanishi hali ya baridi inatarajiwa,

Endelea Uk 12

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya afrika

Kutoka uk 11

lakini kunakuwa na hali ya baridi kuliko ya kawaida katika Bahari ya

Pacific, kumaanisha mabadiliko ya hali ya hewa ulimwenguni. Eneo la Kusini mwa Afrika lina joto zaidi na ukavu, huku Mashariki ya Afrika ikiwa na baridi na yenye mvua wakati wa El Niño, maeneo yote mawili yakiwa na athari kubwa tofauti zilizo kinyume na kila moja.

Wakati wa matukio ya La Niña, Afrika Mashariki huwa kame na yenye joto huku Kusini mwa Afrika ikiwa na mvua na baridi wakati wa kipindi cha joto cha Kusini mwa ulimwengu. Kwa kawaida La Niña huchukua kati ya miezi 6 na 24. Tangu 1950, kumekuwa na matukio ya El Niño 24 na La Niña 17, kumi yakitokea punde tu baada ya mwaka wa El Niño. Hali ya sasa ya La Niña inaweza kuendelea hadi mwanzoni mwa 2023.

Mwisho wa kipindi cha joto unatarajiwa kuwa na La Niña, mbaya zaidi, kikiwa na mvua kubwa kuliko kawaida sehemu nyingi za kusini mwa bara; utabiri unaonyesha kuwa sehemu ya mwisho ya msimu itakuwa na mvua kubwa.

Lakini raia wa Afrika Kusini tayari wamekuwa wakipitia visa vya matukio ya mabadiliko ya tabia nchi, ambayo yanaonekana kuhusishwa na hali ya ENSO, yasiyo ya kawaida, kila moja ikisababisha kimbuga kinachozua uharibifu, na kutupa maji mengi katika kipindi kifupi sana, kusababisha mafuriko yanayoandamana na vifo. Hali hii huwa na baridi kali (mara nyingi ikitoka baharini) ambapo upepo mkubwa "unakatwa" kutoka mawimbi ya kawaida ya upepo unaovuma kutoka magharibi.

# Maafa makuu ya tukio la La Nina

Hii inatokea wakati hewa ya juu inajitenga na kutembea pole pole na kuvutia unyevu wa bahari na hewa iliyojaa unyevu ya maeneo yaliyo kwenye Tropiki, ikiwa nchi kavu. Kukutana kwa hewa hii kunasababisha matukio makubwa yanayodumu kwa saa chache lakini yanayosababisha uharibifu mkubwa, hasa kupitia mafuriko ya ghafla yanayobadilika kuwa vijito vinavyoelekea mito inayojaa uchafu wa kila aina na vifusi.

Ingawa mifumo hubakia, mvua huendelea na kusababisha mafuriko makubwa na uharibifu. Kuna mjadala kuhusu hasa uhusiano wa mabadiliko ya tabia nchi ulimwenguni na msururu wa kile wataalamu wa mabadiliko ya tabia nchi wanakiri ni hali 'nadra' lakini ambayo imekuwa ya kawaida.

Afrika Kusini ilikumbwa na matukio mabaya kama hayo Aprili, mawili zaidi, (au moja refu zaidi katika mikumbo miwili) yakikumba sehemu kubwa ya nchi siku za hivi majuzi, na moja kama hayo ikitarajiwa kutokea Pwani na kuelekea kutua jimbo la Western Cape wikendi hii.

Sehemu hii ya nchi ilikuwa imeanza kukauka kutokana na tukio lisilo la kawaida ambalo lilisababisha uharibifu mkubwa wikendi iliyopita, hasa karibu na Johannesburg, na kusababisha vifo vya watu 14 kwa kusombwa na maji wakati mmoja huku wengine wakikosa kupatikana. Katika maeneo mawili ya kusini na magharibi ya nchi, na maeneo ya kati ya milima ya nyanda za juu ya Johannesburg, kujirudia kwa matukio hayo kumesababishia jamii uharibifu na shida kwa watu maskini zaidi na wasioweza kustahimili madhara kama haya.

Katika sehemu za Soweto, nyumba na barabara zilisombwa na matukio ya hivi majuzi ya hali ya anga, huku mitaa ya mabanda iliyo nyanda za chini mijini ikisombwa, mamia ya watu kupoteza makao, bidhaa, stakabadhi, pesa na mali yao yote.

Pia kulikuwa na uharibifu mkubwa katika miundomsingi, huku laini mbili za barabara moja kuu Johannesburg zikisombwa na stima na maji safi kwa maelfu ya watu kukatizwa bila dalili za kupatikana hivi karibuni.

Watu zaidi ya 300 waliokolewa kutoka eneo moja Soweto, kabla ya kutokea tena kwa hali hiyo iliyotarajiwa. Katika jimbo la Western Cape, watu

1,500 wanahitaji msaada wa dharura, linasema shirika la kibinafsi la Gift of the Givers. Wengine wengi wanatarajiwa kuwa hatarini kama hali inayotarajiwa itatokea kikamilifu.

Matukio ya awali yasiyotarajiwa ya hali ya anga yamekuwa yakisababisha mafuriko makubwa na kusababisha uharibifu kote Afrika Kusini. Mnamo Aprili mwaka huu, mvua ya siku nyingi jimbo la KwaZulu-Natal eneo la kusini mashariki ya Afrika Kusini yalizua mafuriko yaliyoleta uharibifu wa kihistoria, hasa karibu na mji wa Durban, huku vifo 435 vikirekodiwa, wengi kuorodheshwa kuwa 'waliopotea' na uharibifu mkubwa kwa maelfu ya nyumba na miundomsingi muhimu zikiwemo barabara kuu na mifumo ya uchukuzi, mawasiliano na stima.


Usambazaji wa maji safi katika baadhi ya maeneo yaliyoathiriwa bado haujarudishwa. Tukio hili lilikuwa moja la majanga mabaya zaidi katika Afrika Kusini kufikia sasa katika karne hii, lilisababisha hasara ya dola za Amerika1.57 bilioni na lilifaa kutangazwa kuwa janga.

Sehemu ya Laingsburg, mji mkubwa wa kilimo ulio magharibi mwa jimbo la Western Cape karibu na eneo kame la Great Karoo, iliharibiwa na mafuriko mnamo 1981, ambayo pia yalisababishwa na hali sawa.

Katika tukio hilo, watu 104 walikufa huku mili 32 pekee ikipatikana. Ni nyumba 21 kati ya 184 katika sehemu iliyokumbwa na mafuriko ambazo hazikuathiriwa huku mali nyingine zikiharibiwa kabisa au kiasi cha kutorekebishwa.

Huku tukio lingine likitarajiwa na likielekea pwani ya kusini magharibi ya Afrika Kusini, maafisa wanasema wamejiandaa kwa awamu nyingine ya mafuriko yanayosababisha janga. Hali hii inatarajiwa kutokea Ijumaa hadi Jumamosi, huku Huduma ya Hali ya Hewa ya Afrika Kusini tayari ikiwa imetoa onyo la kutokea kwa mafuriko na hali mbaya ya hewa katika kipindi hicho.

*- Imetafsiriwa na Benson Matheka*




Ramani ya hali ya hewa iliyotolewa na Shirika la Huduma za Hali ya Hewa Afrika Kusini inaonyesha kimbunga kikiendelea kushika kasi katika pwani ya kusini-magharibi ya Afrika na kutishia kusababisha mvua nyingine hatari na yenye uharibifu mkubwa nchini Afrika Kusini na maeneo jirani.

ePaper Copy Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# kurunzi ya dunia

SULUHU YAFIKIWA KATIKA COP-15

# MKATABA WA AMANI NA ASILI



Waziri wa Tabianchi na Mazingira wa Norway, Espen Barth Eide (katika) na wajumbe wengine wakipongeza wakati wa kikao kikuu cha Mkutano wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Viumbe Asili COP15) jijini Montreal, Canada, mnamo Desemba 19. PICHA I AFP

## Rais Joe Biden aunga mkono mkataba na kubuni mpango wa '30 kwa 30' nchini ingawa Amerika si mshirika wa kongamano

• Montreal

Nchi zilifikia mkataba wa kihistoria Jumatatu kukabiliana na uharibifu wa mazingira wa miongo kadhaa ambao umetishia viumbe asili na mazingira.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres ametaja hatua hiyo kuwa "mkataba wa amani na viumbe asili."

Mkutano wa viongozi wa COP 15 kuhusu viumbe hai jijini Montreal ulipoelekea ukingoni, mwenyekiti wake, Waziri wa Mazingira wa China, Huang Runqui, alitangaza kufikiwa kwa mkataba huo kwa kugonga nyundo yake, iliyotoa sauti kubwa.

"Hatimaye tunaanza kupalilia mkataba wa amani na viumbe asili," Bw Guterres akasema akipongeza mkataba huo.

Mkuu wa Umoja wa Ulaya (EU) Ursula von der Leyen alisema mkataba huo ni "msingi wa hatua ya dunia kuhusu viumbe hai, unaoongezea Mkataba wa Paris Kuhusu Hali ya Anga."

Amerika ilipongeza matokeo hayo ikiyataja kuwa "hatua muhimu" na kupongeza hatua iliyochukuliwa na hasidi wake, China. Msemaji wa Wizara ya Mashauri ya Kigeni Amerika, Ned Price, alitaja mkataba huo kuwa "wenye mambo mengi mazuri."

Rais wa Amerika, Joe Biden, anaunga mkono mkataba huo na amezindua mpango wake wa "30

Endelea Uk 14

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

kurunzi ya dunia

# Maafikiano kuhusu mazingira

Kutoka uk 13

kwa 30"nchini humo.

Lakini Amerika si mshirika rasmi wa mkataba huo wa viumbe asili kwa sababu ya upinzani kutoka kwa wanachama wa Republican katika bunge la Congress.

Baada ya miaka minne ya mazungumzo makali, zaidi ya nchi 190 ziliunga mkono mkataba huo uliofikiwa kwa usaidizi wa China, ukilenga kuokoa nchi kavu, bahari na viumbe asili kutokana na uchafuzi, uharibifu na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

"Tuna mpango ambao nafiriki unaweza kutuongoza kufanya kazi pamoja kuzuia kupotea kwa viumbe asili, kuweka viumbe asili katika mkondo wa ufufuzi kwa manufaa ya watu wote duniani," Huang akaambia mkutano huo.

Mkataba huo unaahidi kukomboa asilimia 30 ya dunia kuwa eneo linalolindwa kufikia 2030, kutoa msaada wa dola 30 bilioni (Sh360 bilioni) wa kufadhili shughuli za uhifadhi katika mataifa yanayoendelea na kukomesha tishio zinazokabili viumbe mbalimbali.

Wanamazingira wamelinganisha mkataba huo na mpango mkubwa kwa kupunguza ongezeko la joto hadi kima cha 1.5 C, chini ya mkataba wa Paris. Hata hivyo, wengine walionya kuwa mkataba huo hauna masuala yote yanayohitajika.

Brian O'Donnell wa shirika la "Campaign for Nature" aliutaja kuwa "hatua kubwa zaidi ya kutunza ardhi na bahari katika historia." "Kongoni, kasa wa baharini, kasuku, kifaru, miti ya kiasili, vipepeo, samaki aina ya mwali na pomboo ni miongoni mwa mamilioni ya viumbe asili ambao watapata matumaini ya kunawiri mkataba huu ukitekelezwa kikamilifu," akaongeza O'Donnell.

Mkataba huo unaahidi kulinda haki za watu asili kama walinzi wa ardhi zao, mojawapo ya masuala ambayo waendesha kampeni wanataka yatekelezwe.

Lakini wadadisi wanasema mkataba huo una upungufu katika nyanja zingine kwani unahimiza biashara mbalimbali kuripoti athari zake kwa viumbe asili badala ya kuzipa wajibu wa kufanya hivyo.

Malengo 23 katika mkataba huo pia yanajumuisha kuokoa mamia ya mabilioni ya dola kwa kupunguza ruzuku za kilimo zenye madhara kwa mazingira, kupunguza hatari kutoka kwa kemikali za kuua wadudu na kupambana na viumbe hatari.

Wakati fulani mazungumzo yalionekana kuelekea kuvurugika nchi zilipogombana kuhusu pesa. Kiasi cha pesa ambazo nchi tajiri zitatuma kwa nchi zinazoendelea, ambako kunapatikana vingi vya viumbe asili, kiliibuka kuwa suala kuu. Nchi zinazoendelea zilipigania kuundwa kwa hazina mpya kubwa ya msaada kutoka Nchini za Kaskazini.

Lakini badala yake, kielelezo cha mkataba huo kilipendekeza kuwa muafaka ufikiwe wa kuunda hazina chini ya Shirika la Mazingira Ulimwenguni (GEF). Suala hilo liliibuliwa na DRC, ambako kuna utajiri mkubwa wa viumbe asili.

Msaada wa kifedha unaotolewa kwa nchini zinazoendelea kufadhili shughuli za kulinda viumbe asili ni karibu dola 10 bilioni (Sh1.2 trilioni) kila mwaka.

Mjumbe wa DRC aliongea ukumbini kutaka ufadhili wa kila mwaka uongezwe hadi dola 100 bilioni (Sh12 trilioni lakini Huang alitangaza kuwa mkataba huo umepitishwa, hatua iliyoudhi wajumbe wa DRC. — *AFP*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*



Waziri wa Mazingira wa China Huang Runqiu akizungumza na Makamu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri wa Mazingira wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Eve Bazaiba Masudi, kabla ya kikao kikuu cha mkutano jijini Montreal, Quebec, mnamo Desemba 19. PICHA I AFP

# Maana hasa ya mkataba kuhusu viumbe asili

• Montreal

Baada ya miaka ya majadiliano, ulimwengu umekubaliana kuhusu mkataba muhimu wa kulinda viumbe wanaoangamia na mazingira.

Haya ni baadhi ya mafanikio ya mkataba huo uliofikiwa katika mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN) jijini Montreal kwa jina COP-15, na pia mapungufu yake.

Nguzo kuu ya mkataba huo ni kilichotajwa kuwa lengo la "30 kwa 30" – ahadi ya kulinda asilimia 30 ya ardhi na bahari ifikapo 2030 -- kutoka kiwango cha sasa cha karibu asilimia 17 ya ardhi na asilimia saba ya bahari.

Malengo ya bahari yaliripotiwa kupingwa na baadhi ya nchi lakini yalijumuishwa katika nakala ya mwisho. Baadhi ya wataalamu walikuwa wamesema asilimia 30 ni lengo la chini, wakisisitiza kuwa ni bora kulinda eneo la ukubwa wa asilimia 50.

Haki za kiasili zilishughulikiwa kote katika nakala hiyo -- ukilinda haki za kiasili za watu kusalia walinzi wa ardhi wanazotumia na kuhakikisha kuwa hawafurushwi kwa kizingizio cha uhifadhi.

Shirika la Kimataifa kuhusu Viumbe Asili lilipongeza mkataba huo kwa "kusisitiza kuheshimu haki za Watu Asilia na jamii zingine za maeneo husika."

Mkataba huo unaidhinisha lengo la kuhimiza nchi tajiri kutoa "angalau dola 20 bilioni za Amerika kufikia 2025 na ... angalau dola 30 bilioni kwa mwaka, karibu maradufu na mara tatu ya kiwango cha sasa cha msaada wa kimataifa kwa viumbe asili.

Unataka watu wapate manufaa kutokana na "rasilimali za kijenetiki" kutoka kwa nchi zao: mali ya kiasili, kama vile dawa au viungo vya kosmetiki katika mimea inayoweza kupatikana katika nchi inayoendelea lakini habari zake za kijenetiki zitambuliwe na kutolewa kwa watafiti na kampuni za nchi zingine.

Lakini wakereketwa walilalamika kuwa mktaba hauna na "mafanikio" ya kutosha ya kupiga hatua bora. Kwa mfano, mkataba huo unasema tishio zinazoletwa na binadamu kwa viumbe wanaojulikana lazima zisitishwe, na kufikia 2050 kiwango cha tishio la kuangamia kwa viumbe wote kipungue mara kumi -- lakini hakuna malengo ambayo nchi zinapaswa kufikia kabla ya mwaka huo. — *AFP*

*- Imetafsiriwa na Charles Wasonga*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media

# China yatumia teknolojia ya juu kuzima fujo




• Beijing

Polisi nchini China wameanza kutumia vifaa vya teknolojia ya hali ya juu katika juhudi za kukabili wimbi kali la maandamano nchini humo. Wanatumia teknolojia maalumu ya kutambua watu kwa sura zao na maeneo waliko ili kunasa na kukamata waandamanaji.

Malalamiko mengi yaliibuka nchini kutokana na masharti makali ya serikali kudhibiti kuenea kwa Covid-19. Waandamanaji walikuwa wakishinikiza serikali ifungue upya shughuli za kibiashara na kurudisha uhuru wa kisiasa, hali ambayo haijashuhudiwa nchini humo kwa miongo mingi.

Serikali ilipotangaza msako mkali dhidi ya waandamanaji hao, maafisa wa usalama walianza operesheni, wakitumia mitambo hiyo kunasa waandamanaji, kulingana na wakili mmoja wa masuala ya haki za binadamu anayetoa ushauri wa kisheria kwa waandamanaji hao bila malipo.

"Katika miji ya Beijing, Shanghai na Guangzhou, polisi wamekuwa wakitumia teknolojia ya hali ya juu," akasema Wang Shengsheng, wakili anayehudumu katika jiji la Zhengzhou. "Katika miji mingine, inaonekana wamekuwa wakitegemea video kutoka kwa mitambo hiyo na mfumo wa kutambua sura," akaambia AFP.

Inawezekana polisi jijini Beijing walitumia data za simu kujua watu waliko zilizonaswa na kwa mitambo hiyo au namba maalumu za Covid kutoka kwa watu waliokuwa wakiabiri teksi kuelekea maeneo ambako maandamano hayo yalikuwa yakiendelea, akasema.

— *AFP*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

# UFARANSA KUBORESHA MLO MUHIMU WA CHINA



• Ufaransa

Katika shamba moja la kufuga samaki karibu na mji wa Bordeaux, Christophe Baudoin anaendesha mashine ya kupiga picha ndani ya viumbe katika tumbo la samaki aina ya sturgeon kukagua mayai yake. "Caviar!" anasema kwa sauti ya juu huku mashine hiyo ikionyesha mwanga karibu na kila yai dogo.

"Imekua kupita kiasi!" anasema tena, akionyesha kuwa ujauzito wa samaki huyo umekaa sana na mayai yamekuwa mepesi - yamepoteza ngozi yake muhimu. Atarudi ziwani kungoja kipindi kingine katika miaka miwili.

Kwa kampuni ya Sturia, huo ni mchakato mrefu sana - wanapiga picha samaki 20,000 kwa mwaka ili kupata tani 300 za chakula aina ya caviar – lakini mabadiliko ya tabia nchi yamefanya shughuli hiyo kuwa muhimu.

Samaki wengi wanavuliwa wakiwa "wamekomaa kupita kiasi" kwani kiwango cha juu cha joto majini kimefupisha muda wake wa kupata mimba.

Kwa watu wanaosimama ndani ya maji wakichukua samaki hao wakubwa ili kukaguliwa, hawatamani siku za msimu wa baridi, barafu ya sentimita kumi (inchi nne) ilipofunika maziwa. Lakini mabadiliko hayo bado yanashangaza. "Ni miaka kumi tangu tuone barafu yoyote katika maziwa haya," akasema Baudoin.

Samaki mmoja kati ya watano walikufa 2021 kiwango cha joto katika maji kilipofikia nyuzijoto 30, nyuzijoto tano zaidi ya kiwango wanachohitaji samaki hao. Kutokana na kupungua baharini - ikiwemo Bahari ya Capsian, Urusi na Iran - samaki aina ya sturgeon sasa hupatikana tu katika mashamba ya kufugia samaki, mengi yakiwa China.

Samaki hao walikuwa wakivuliwa katika Mto Gironde nchini Ufaransa kwa karne nyingi, lakini mayai yao yalikuwa yakipewa watoto, wazee na nguruwe hadi matajiri kutoka Urusi waliokuwa wakitoroka maasi ya Kikomunisti karne moja iliyopita walipowaonyesha wenyeji umuhimu wake.

Yaligeuka chakula muhimu jijini Paris baada ya wahamiaji kutoka Armenia, Melkoum na Mouchegh Petrossian, kushawishi Hotel Ritz jijini humo iwapikie mchuzi wa caviar katika miaka ya 1920.

Ufugaji wa samaki hao ulianza nchini humo katika miaka ya 1990, lakini kwa kuwa inachukua miaka kumi kumlea samaki mmoja wa sturgeon, mchakato huo huwa mrefu sana na wa kuchosha.


Ufaransa imeshindwa kuifikia China katika uzalishaji wa idadi ya juu wa samaki hao na sasa wakulima wake wameegemea uboreshaji wa kiwango cha samaki wanaofuga.

Dulalu alisema sasa wanataka kuboresha caviar kutokana na kupungua kwa idadi ya samaki baharini. "Lengo kuu ni kuzalisha kiasi kidogo lakini bora," akasema. "Watu watakuwa wakila kiasi kidogo kwa kuwa bei yake ni ghali, lakini itakuwa vizuri kwani wataridhika."

"Hatuwezi kuwa namba moja katika uzalishaji, lakini tunaweza kuongoza katika ujuzi na sayansi." — *AFP*

*- Imetafsiriwa na Wanderi Kamau*

ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media Group "ePaper Copy" Nation Media



SPORT ON!
JAMES WOKABI
BERNARD NDONG
HOSTS
NATIONFM 96.3 FM
WHERE GOOD MUSIC LIVES
SATURDAYS 3PM